

Kwa nini watu wanawekewa mashine za kuwasaidia kupata oksijeni wakati hewa ipo hata pale walipo?

Ooh! kumbe huwenda shida sio upungufu wa oksijeni, ila ni viungo vya mwili vinavyohusika na mambo ya mfumo wa upumuaji haviwezi kufanya kazi vizuri.

Kuhusu watu kusema fursa hazionekani huwenda ni changamoto ya tafasiri, na sio kwamba fursa hazipo kiuhalisia.

Tatizo si ukosefu wa fursa.

Tatizo ni ukosefu wa macho ya kuona fursa.

Tatizo ni ukosefu wa mfumo wa kuzigeuza fursa zilizokuwa katika hali dhania kuwa uhalisia.

Kitabu hiki nimekiandaa kwa ajili ya watu wanaotaka kujifunza ufundi wa kuona, kutengeneza na kuzitumia fursa tulizonazo kwenye mazingira yetu.

*“Watu wengi hawajakosa nguvu na akili, ila wanakosa mfumo wa kubadilisha nguvu na akili zao kuwa mashine za kuzalisha yale wanayotamani kuyaishi.”*